

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE

08 JUNI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 08 JUNI, 2017

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka 2017/2018 (*Monetary Policy Statement for the Year 2017/2018*).

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**360. MHESHIMIWA MAIDA HAMAD ABDALLAH
(VITI MAALUM):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaamua kurudisha fedha zilizokusanywa na Halmashauri kupitia vyanzo vyake vya ndani ili ziweze kutekeleza majukumu yake na mikakati iliyopangwa kwa ufanisi.

361. MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni kwa nini Serikali iliamisha Madaktari saba kwa mara moja kutoka Hospitali ya Wilaya ya Bukombe huku ikijua Wilaya ya Bukombe ina upungufu mkubwa wa Madaktari.



WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

362. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kuanzisha miradi mikubwa na midogo ya maji:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni miradi gani mikubwa na midogo iliyokamilika na isiyokamilika katika Jimbo la Nyang'hwale;

(b) Je, kama kuna miradi ambayo haijakamilika mpaka hapo ilipofikia imetumia fedha kiasi gani;

(c) Je, ni lini sasa miradi hiyo itakamilishwa katika Jimbo la Nyang'hwale.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

363. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Tanzania ni moja kati ya Nchi Wanachama wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini Wenyewe kwa Vigezo vya Utawala Bora (APRM):-

Je, Serikali imejitathmini kwa kiasi gani katika dhana nzima ya Demokrasia na Utawala Bora, Utawala wa Kisiasa, Usimamizi wa Uchumi na Maendeleo ya Kijamii.


IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

SAA 10.00 JIONI

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.



DODOMA
08 JUNI, 2017

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE